# IKULU ZANZIBAR

SERIKALI KWA MAENDELEO YA WANANCHI

TOLEO NO. 031 ISSN 1821 - 8253 JANUARI 2017

# ZANZIBAR YAADHIMISHA MIAKA 53 YA MAPINDUZI




Website: www.ikuluzanzibar.go.tz / Email: info@ikuluzanzibar.go.tz / Twitter: Zanzibarupdates / Facebook: Zanzibarupdates

## Bodi ya Wahariri

**Mhariri Mkuu**
Hassan K. Hassan

**Mhariri Msaidizi**
Haji M. Ussi

**Waandishi**
Rajab Y. Mkasaba
Said K. Salim
Yunus S. Hassan
Amina M. Ameir

**Mpiga Picha**
Ramadhan O. Abdalla

**Msanifu**
Aziz I. Suwed

## UTAMBULISHO

Wapenzi wasomaji wa Jarida la Ikulu tunafuraha kukukaribisheni katika uendelezaji wa juhudi za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuimarisha mawasiliano na wananchi.

Ni lengo la Ofisi ya Rais kukuza mawasiliano na wananchi kwa kutumia njia tofauti kama vile Jarida, vipeperushi pamoja na vyombo vyengine vya habari.

Tunakaribisha maoni yenu ili tuweze kufikia lengo hilo.

Jarida hili limetolewa na Idara ya Mawasiliano Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

P.O.BOX: 2422
Zanzibar - Tanzania
Phone: +255 223 0814/5
Fax: 024 223 3722
Email: info@ikuluzanzibar.go.tz
Website: www.ikuluzanzibar.go.tz
Twitter: Zanzibarupdates
Facebook: Zanzibarupdates

# MAONI YA MHARIRI

## Yaoneni mafanikio ya Mapinduzi

Mwenye macho haambiwi tazama ni msemo wa wahenga ambao kama ilivyo misemo mingine ya Kiswahili unabeba maana pana katika jamii na unaweza kutafsiriwa kwa matukio na hali tofauti.

Katika mtazamo wa maendeleo msemo huu unaelekezwa kwa wale wenye kubeza mafanikio yaliyopatikana serikalini hasa baada ya Mapinduzi matukufu ya tarehe 12 Januari 1964 ambapo wananchi wa Zanzibar chini ya Jamadari Mkuu wa Mapinduzi Marehemu Mzee Abeid Amani Karume waliamua kukata minyororo ya utumwa na kukandamizwa kwa kunyimwa haki za msingi za kiuchumi na kijamii.

Ni ukweli uliowazi kwamba mafanikio makubwa yamepatikana katika kipindi cha miaka 53 iliyopita katika kuimarisha sekta za uchumi, siasa na jamii ikilinganishwa na zaidi ya miaka 200 ambapo Zanzibar iliendeshwa chini ya utawala wa wageni.

Hali ya kuimarika kwa uchumi sambamba na kuimarika kwa huduma bora za jamii zimekuwa zikionesha kuwa bora zaidi kila siku zinapoendelea jambo ambalo linatosha kuthibitisha kuimarika kwa maisha ya watu wa Zanzibar.

Kwa mfano ukuaji wa uchumi mwaka uliopita tu, unaonekana kuwa tofauti na mwaka uliotangulia. Ni dhahiri hali hiyo inaimarisha ubora wa upatikanaji wa huduma za jamii mjini, vijijini, Unguja na Pemba.

Katika hotuba yake aliyoitoa kwenye kilele cha maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi ya Zanzibar Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, alisema bayana kwamba katika kipindi cha Januari hadi Novemba 2016, mapato yaliyokusanywa kutokana na vyanzo vya ndani, yaliongezeka kutoka TZS bilioni 336.6 mwaka 2015 hadi TZS bilioni 441.3 mwaka 2016. Kiasi hicho ni ongezeko la TZS bilioni 104.7, sawa na asilimia 31.1. Kadhalika, katika kipindi hicho, Serikali imepokea jumla ya TZS bilioni 54.53 kutoka kwa Washirika wetu wa Maendeleo, kuanzia mwezi wa Januari hadi Oktoba, 2016.

Mapato hupimwa na matumizi. Kwa upande wa matumizi, Serikali imetumia jumla ya TZS bilioni 436.6 kwa kipindi cha Januari hadi Oktoba 2016. Kwa jumla, katika kipindi hicho, Mapato ya Serikali yalipindukia matumizi kwa jumla ya TZS bilioni 4.7, sawa na ongezeko la asilimia 1.08. Haya ni mafanikio makubwa katika usimamizi wa fedha za umma.

Hii inatokana na mafanikio ya jitihada za Serikali za kudhibiti matumizi yasiyokuwa ya lazima ya fedha za umma na badala yake kuelekeza matumizi hayo kwenye huduma muhimu za kijamii ikiwemo afya, maji safi na salama, elimu na nyenginezo ambazo mafanikio yake pia yanaonekana wazi wazi Unguja, Pemba, mjini na vijijini.

Katika kipindi hiki, Serikali iliidhinisha jumla ya miradi 51 ya uwekezaji, yenye thamani ya USD milioni 497.92. Katika miradi hiyo, asilimia 53 ni miradi inayomilikiwa na wawekezaji wazalendo. Miradi hii inatarajiwa kutoa ajira zipatazo 2,658 na hivyo inakwenda sambamba na azma ya Serikali ya kupunguza tatizo la ajira, na hatimae kupunguza umaskini.

Mafanikio hayo hayako kwenye nadharia bali yanaonekana dhahiri kwa macho katika kila eneo. Kwa mfano inapozungumziwa kuimarisha uwekezaji, katika kipindi cha 2015/16, Serikali kwa kushirikiana na Kampuni ya SS Bakhresa imeanza ujenzi wa miundombinu ya mji mpya wa kisasa – "Fumba Bay Satelite City", uliopo Fumba katika eneo la EPZ.

Kadhalika, nyumba za kisasa 150 kati ya 500, tayari zimeanza kujengwa kwenye Mradi wa "Uptown living" unaoendeshwa na Kampuni ya "Union Property Developers". Mji mpya wa kisasa wa "Fumba Bay Satelite City" na mradi wa nyumba mpya 150 "Uptown Living" zikiwa kwenye hatua mbali mbali za ujenzi.

Vile vile, mradi wa ujenzi wa nyumba za kisasa katika eneo la Nyamanzi umeanza kutekelezwa katika kipindi hiki. Hadi hivi, sasa nyumba 20 kati ya nyumba 1300 zimeanza kujengwa na zimefikia katika hatua mbali mbali.

Hii ni miradi michache tu kati ya mingi ambayo serikali imeifanikisha na mafanikio yake yanaonekana wazi wazi.

Ni bahati mbaya sana kwamba wapinga maendeleo hawayaoni mafanikio hayo pamoja na kuruzukiwa macho na Mwenyezi Mungu. Ni kweli mwenye macho haambiwi tazama.

# Zanzibar Yaadhimisha Miaka 53 ya Mapinduzi



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alipokuwa akipokea salamu ya heshima ya Gwaride la Vikosi vya Ulinzi katika sherehe za Kilele cha Maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi Zanzibar zilizofanyika katika Uwanja wa Amaan, tarehe 12 Januari, 2017

Mamia ya wananchi wa Zanzibar wameshiriki katika kilele cha Maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari, 1964, tarehe ambayo wataendelea kuikumbuka katika maisha yao yote kutokana na kujikomboa kutoka katika madhila makubwa ya kutawaliwa na kunyimwa mahitaji muhimu ya kijamii wakiwa kwenye ardhi yao.

Katika hotuba yake kwenye maadhimisho hayo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alibainisha mafanikio makubwa yaliyopatikana tokea baada ya Mapinduzi hayo hasa katika kuimarisha huduma za kijamii kwa wananchi wa Zanzibar bila ya ubaguzi.

"Leo ni siku muhimu sana katika historia ya wananchi wa Zanzibar, ambapo miaka 53 iliyopita tuliikata minyororo ya utawala wa Kisultani na ukoloni wa Kiingereza uliodumu kwa takriban miaka 132. Wananchi walikataa kwa vitendo kudharauliwa, kunyanyaswa, kubaguliwa na kutokuheshimiwa katika nchi yao. Chama cha Afro-Shirazi, kiliongoza vuguvugu la kuikomboa Zanzibar, dhidi ya madhila ya wakoloni, mabwanyenye na mabepari" Alisema Dk. Shein.

Katika kuadhimisha sherehe hizo, wananchi huzitumia sherehe hizo kuwakumbuka na kuwashukuru wazee Waasisi wa Chama cha Afro-Shirazi walioongozwa na Rais wake wa Kwanza, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume.


Daima viongozi hao hawatosahaulika kutokana na ushujaa wao na ushindi wa jitihada zao za kupigania haki, kuleta usawa na maelewano na kuondoa pingamizi zote walizokuwa wakizipata wananchi wa Unguja na Pemba.

Ni ukweli ulio wazi kwamba Mapinduzi hayo ya tarehe 12 Januari 1964, ndiyo yaliyowainua wanyonge,

yameleta uhuru wa kweli na yamesimamisha utawala wao katika misingi ya usawa na haki. Ni kutokana na Mapinduzi, ndipo Wafanyakazi na Wakulima wa Zanzibar walipoirudisha heshima na ubinadamu wao katika nchi yao.

Fahari kubwa ya wananchi wa Zanzibar katika kusherehekea miaka 53 ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kushuhudia kuwa katika kipindi cha miaka 53 ya Mapinduzi, wanaendelea kusherehekea sikukuu hiyo wakiwa katika hali ya amani, umoja, mshikamano wakijivunia mafanikio makubwa ya maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.


Viongozi wakiwa wamesimama wakati wimbo wa Taifa ukiimbwa


Mgeni rasmi Dk. Ali Mohamed Shein akikagua gwaride rasmi


Kikosi cha FFU Wanaume


Kikosi cha JWTZ Wanaume


Kikosi cha KMKM Wanaume


Kikosi cha JWTZ Wanawake


Kikosi cha JKU Wanawake


Kikosi cha POLISI Wanawake


Maandamano ya Wananchi


Maandamano ya Vijana

# Mafanikio ya juhudi za kuimarisha sekta ya uwekezaji Zanzibar yameanza kuonekana



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk .Ali Mohamed Shein akifungua pazia kuashiria uwekaji wa jiwe la msingi ujenzi wa VERDE-MARINE HOTEL Mtoni Mjini Magharibi,hoteli ya kisasa yenye hadhi ya nyota 5 inayojengwa na kampunui ya ujenzi ya Bakhresa Group of Companies,ikiwa ni katika shamra shamra za miaka 53 ya Mapinduzi ya Zanzibar, tarehe 03 Januari, 2017. Kulia ni Mwenyekiti wa Bakhresa Group of Companies Bw. Said Salim Bakhresa

Harakati za ujenzi wa majengo ya kisasa sambamba na upanuzi wa miji mipya katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba zimeanza kuleta muonekano mpya wa Zanzibar mambo ambayo yanaongeza matumaini kwa wananchi wa Zanzibar hasa wapenda maendeleo kwa kuuona wazi wazi muelekeo wa kuwa na Zanzibar mpya tuitakayo.

Umuhimu wa kuwa na maeneo huru ya kiuchumi Zanzibar ulianza kuonekana tokea mwanzoni mwa miaka ya 90 wakati Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya uongozi wa Dk. Salmin Amour ilipoamua kutenga eneo la Fumba, Amani na Maruhubi kwa Unguja na Micheweni kwa Pemba kuwa ni maeneo huru ya uchumi.

Chini ya mpango huo wa muda mrefu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilidhamiria kuwashajihisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuja kuwekeza kwenye maeneo hayo. Hata hivyo, utekelezaji wa mpango huo ulichukua muda mrefu kutokana na hali isiyoridhisha ya ukusanyaji wa mapato ambao ulipelekea kasi ndogo ya ukuaji uchumi.

Maeneo hayo hayakuwa yamejengewa miundombinu ya uhakika ambayo ingeweza kuwashawishi wawekezaji kuekeza miradi yao. Ili kuongeza kasi ya uwekezaji, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba tokea ilipoingia madarakani imekuwa ikichukua juhudi maalum kuhakikisha kuwa maeneo hayo yanaendelezwa. Serikali iliidhinisha jumla ya miradi 51 ya uwekezaji, yenye thamani ya USD milioni 497.92. Katika miradi hiyo, asilimia 53 ni miradi inayomilikiwa na wawekezaji wazalendo. Miradi hii inatarajiwa kutoa ajira zipatazo 2,658 na hivyo inakwenda sambamba na azma ya Serikali ya kupunguza tatizo la ajira, na hatimae kupunguza umaskini.



Miongoni mwa nyumba za kisasa zinazoendelea kujengwa katika mradi wa Ujenzi wa Miundombinu katika maeneo huru ya Uchumi huko Fumba Wilaya ya Magharibi "A" Mkoa Mjini Magharibi , sambamba na uwekaji wa jiwe la msingi nyumba za kuishi zilizozinduliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein ikiwa ni shamra shamra za maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, tarehe 03 Januari, 2017

Lakini ili kuongeza mchango wa sekta binafsi katika kukuza uchumi wa Zanzibar, SMZ imepanga kusimamia utekelezaji wa sera, mwongozo na sheria ya ushirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi sambamba na kuharakisha miradi yenye tija inayopendekezwa kufanyika.

Aidha, serikali ilipanga kukamilisha utekelezaji wa uendelezaji wa mji mpya wa kisasa katika maeneo huru ya uchumi ya Fumba na Micheweni na kuweka vivutio kwa wewekezaji wa sekta ya viwanda.

Pamoja na hatua hizo, Serikali pia imepanga kuweka mazingira endelevu ya kuwawezesha kimtaji wawekezaji wa ndani na kuwaunganisha na wawekezaji wa nje pamoja na kuvishawishi vyombo vya fedha kuwapatia mikopo yenye riba na masharti nafuu wawekezaji.

Kutokana na mipango hiyo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inajivunia mwanzo wa mafanikio ya wazi wazi ya juhudi hizo kufuatia uanzishwaji wa miradi mikubwa katika kijiji cha Fumba na kampuni inayomilikiwa na muekezaji mzalendo kampuni ya S S Bakhresa inayojenga nyumba na mji wa kisasa.

Katika kipindi cha 2015/16, Serikali kwa kushirikiana na Kampuni hiyo imeanza ujenzi wa miundombinu ya mji mpya wa kisasa (Fumba Bay Satelite City) katika eneo la EPZ. Kadhalika, nyumba za kisasa 150 kati ya 500, zimejengwa kwenye Mradi wa "Uptown living" unaoendeshwa na Kampuni ya "Union Property Developers". Mji mpya wa kisasa wa "Fumba Bay Satelite City" na mradi wa nyumba mpya 150 "Uptown Living" zikiwa kwenye hatua mbali mbali za ujenzi zimewekewa mawe ya msingi tarehe 9 Januari, 2017 na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein.

Vile vile, mradi wa ujenzi wa nyumba za kisasa katika eneo la Nyamanzi umeanza kutekelezwa katika kipindi hiki. Hadi hivi, sasa nyumba 20 kati ya nyumba 1300 zimeanza kujengwa na zimefikia katika hatua mbali mbali.

Kadhalika, kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Serikali ilianza kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba katika eneo la Mbweni. Mradi huo ni wa ujenzi wa majengo 18 yenye urefu wa ghorofa 7 ambayo yatakuwa na nyumba (Flats) 252. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Novemba 2016, tayari majengo matano yenye jumla ya nyumba 70 za kuishi yalikuwa yameshajengwa. Majengo hayo yanatarajiwa kumalizika mwezi wa Aprili, 2017.

Ujenzi wa hoteli kubwa ya kisasa ya "Verde" (Mtoni Marine) ya nyota tano na vyumba 106, ambao umeanza katika kipindi hiki ni sehemu nyengine inayotia matumaini makubwa ya mafanikio ya utekelezaji wa mpango wa serikali siyo



tu katika kuwakaribisha wawekezaji wa ndani, lakini pia katika kuimarisha sekta ya utalii ambayo nayo imeonesha umuhimu wa pakee katika kukuza uchumi wa taifa. Hoteli hiyo ambayo nayo inajengwa na Kampuni ya SS Bakhressa, iliwekewa jiwe la msingi tarehe 3 Januari, 2017, na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohmed Shein. Ujenzi huo unatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Julai 2017.

Wakati wa sherehe za kuadhimisha miaka 53 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein ile vile alipata fursa ya kuzindua rasmi kiwanda kinachomilikiwa na Makampuni ya Bakharesa kinachoendesha shughuli za uzalishaji wa maziwa cha Azam Dairy Products Ltd kilichoko eneo la Fumba Kororo Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja.

Uzinduzi huo unakwenda sambamba na malengo ya Serikali ambapo, katika kipindi cha pili cha Awamu ya Saba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, lengo ni kuimarisha viwanda ili kupunguza uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi, kuongeza usafirishaji wa bidhaa hizo kwenda nje, kuimarisha utumiaji wa malighafi zinazopatikana nchini na kuongeza ajira kwa wananchi.

Sekta ya Viwanda ilichangia asilimia 19.8 ya Pato la Taifa katika mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 16.8 mwaka 2014. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 3.0.

Katika mwaka 2016, viwanda vitatu vikubwa vya watu binafsi, kiwanda cha maziwa cha Azam, kiwanda cha "Zanzibar Milling Corporation", kilichopo Mtoni na kiwanda cha Sukari kilichopo Mahonda vimeendelea kufanya kazi ya uzalishaji.

Aidha, Kiwanda cha Serikali cha Makonyo ya Karafuu na Viungo vyengine kimeendelea na uzalishaji. Vile vile, Kiwanda cha Matrekta, Mbweni kimefanya kazi ya kuyatengeneza matrekta yote ya Serikali, kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi katika kilimo cha mpunga.

# Pato la taifa linaendelea kukua

Mafanikio ya Serikali katika kukuza pato la taifa yanaendelea kuonekana katika kila eneo kutokana na kukua kwa pato la taifa jambo ambalo linachangiwa na kuimarika kwa miundombinu na huduma za kisasa kwenye vyanzo vikuu vya mapato bandari na huduma kwenye viwanja vya ndege.

Kwa mujibu wa hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwenye kilele cha maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika mwaka wa kwanza wa kipindi hiki cha pili, 2015/2016, cha Awamu ya Saba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inayoongozwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, Serikali imeanza vizuri utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, MKUZA III na



Wafanyakazi wa Kiwanda cha Maziwa cha AZAM DAIRY PRODUCTS LTD wakiwa katika majukumu yao ya kila siku mara baada ya kuzinduliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein wakati alipotembelea Kiwanda hicho huko Fumba Kororo Wilaya ya Magharibi "A" Unguja kuona harakati za uzalishaji, tarehe 05 Januari, 2017

Dira ya Maendeleo 2020 na kupata mafanikio ya kuridhisha katika kuuimarisha uchumi, huduma za jamii na bila ya shaka kujenga misingi imara ya utawala bora.

Katika kipindi hicho, pato halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha wastani wa asilimia 6.6. Pato la mtu binafsi limefikia wastani wa TZS 1,632,000 sawa na USD 817 kwa mwaka 2015. Katika mwaka 2016, kasi ya mfumko wa bei za bidhaa na huduma ilifikia asilimia 6.7 ambapo kasi hiyo ilikuwa asilimia 5.7 katika mwaka 2015. Mfumko wa bei bado umedhibitiwa katika kiwango cha tarakimu moja.

Mafanikio ya kuimarika kwa huduma mbali mbali, yametokana na juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya ukusanyaji wa mapato ambapo kwa kipindi cha Januari hadi Novemba 2016, mapato yaliyokusanywa kutokana na vyanzo vya ndani, yameongezeka kutoka TZS bilioni 336.6 mwaka 2015 hadi TZS bilioni 441.3 mwaka 2016.

Kiasi hicho ni sawa na ongezeko la TZS bilioni 104.7, ambazo sawa na asilimia 31.1. Kadhalika, katika kipindi hicho, Serikali imepokea jumla ya TZS bilioni 54.53 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, kuanzia mwezi wa Januari hadi Oktoba, 2016. Kwa kiasi hicho cha fedha ni dhahiri kwamba washirika wa maendeleo wameendelea kuonesha imani yao kwa Serikali iliyoko madarakani kinyume na matarajio ya wapinga maendeleo.

Akizungumza kwenye kilele cha maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi matukufu ya tarehe 12 Januari 1964, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alitoa pongezi kwa Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya katika kukusanya mapato na amezihimiza taasisi hizo kuendelea na juhudi zao hizo, ili mapato yanayokusanywa kwa kila mwaka yazidi kuongezeka kwa kiwango kikubwa zaidi.

Kwa upande wa matumizi, Serikali imetumia jumla ya TZS bilioni 436.6 kwa kipindi cha Januari hadi Oktoba 2016. Kwa jumla, katika kipindi hicho, Mapato ya Serikali yalipindukia matumizi kwa jumla ya TZS bilioni 4.7, sawa na ongezeko la asilimia 1.08. Hayo ni mafanikio makubwa katika usimamizi wa fedha za umma.

Sifa ya kipekee iliyokwenda Serikalini ni ahadi iliyotolewa na Rais wa Zanzibar ya kuendelea kusimamia vyema matumizi ya fedha hizo na kuwahakikishia wananchi kwamba fedha zinazokusanywa zitaendelea kutumiwa katika kuwahudumia




wananchi kwa mambo muhimu ya maendeleo yao.

Kwa kiasi kikubwa mapato ya serikali kwenye nchi za visiwa kama Zanzibar yanakusanywa kupitia kwenye milango mikuu ya kuingilia kwenye visiwa hivyo ikiwemo kwenye bandari au viwanja vya ndege.

Katika mwaka 2016, Serikali iliendelea na mpango wake wa kuimarisha kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Abeid Amani Karume. Ingawa ujenzi wa jengo jipya la abiria ulisita kutokana na changamoto zilizojitokeza, changamoto hizo zitapatiwa ufumbuzi hivi karibuni na kwamba ujenzi huo unatarajiwa kuendelea mara tu baada ya changamoto hizo kupatiwa ufumbuzi.

Kuhusu uwanja wa ndege wa Pemba, mipango ilitayarishwa ya kufanya upembuzi yakinifu kwa kukipanua kiwanja hicho, ili ndege kubwa za aina ya Boeing 737 - 800 ziweze kutua pamoja na ujenzi wa jengo la abiria jengine. Fedha kwa ajili ya kazi hiyo tayari zimepatikana kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa vifaa vipya vya kufanyia kazi bandarini kwenye sherehe uzinduzi wa vifaa vipya vya kufanyia kazi huko Bandarini ikiwa ni miongoni mwa shamrashamra za miaka 53 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein ameelezea kusikitishwa kwake na tabia ya baadhi ya wafanyakazi bandarini kwa kufanya kazi kinyume na maadili na taratibu za kazi zao na kueleza kuwa endapo wafanyakazi wa aina hiyo watajulikana watashughulikiwa ikiwa ni pamoja na kushtakiwa ama kufukuzwa kazi.

Dk. Shein amelazimika kutoa karipio hilo kutokana na ukweli kwamba juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi wake na harakati za kukuza maendeleo ya uchumi kwa jumla hazitoweza kufanikiwa bila ya kuungwa mkono na kila mwananchi popote alipo.

Ni ukweli uliowazi kwamba wakati Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa awamu zote imekuwa ikitumia njia mbali mbali za kujiimarisha kiuchumi na kimaendeleo, kumekuwa na baadhi ya watu au wafanyakazi wa serikali ambao ama kwa makusudi au kwa bahati mbaya wamekuwa wakijaribu kurejesha nyuma juhudi hizo.

Ili kujidhatiti na mapato ya bandarini, Serikali imo katika matayarisho ya ukamilishaji wa ujenzi wa bandari mpya ya kuhudumia mizigo katika eneo la Mpigaduri. Wakati




Vifaa vipya vya kufanyia kazi Bandarini ikiwemo vifaa vya kuteremshia Makontena ya mizigo mizito inayowasili katika Bandari ya Malindi Mjini Unguja, vimezinduliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika shamra shamra za miaka 53 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, tarehe 04 Januari, 2017

huo huo mipango inaendelea ya kuiimarisha na kuiendeleza Bandari ya Mkoani kwa kuipatia vifaa vya kisasa vya kuhudumia abiria na mizigo.

Kadhalika, Serikali inaendeleza mazungumzo na wawekezaji kwa lengo la kuiimarisha Bandari ya Wete kutokana na umuhimu wake kwa Serikali, wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na watumiaji wote. Kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Serikali itaendelea kuiimarisha gati ya Mkokotoni kwa kukamilisha ujenzi wa jeti kwa ajili ya huduma za usafiri wa wananchi hasa wa Mkokotoni na Tumbatu.



# Matamasha ya biashara yabuni mbinu za kisasa



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na Wajasiriamali kutoka Mkoa wa Mwanza ambao wanafanya bishara ya mikoba na dawa asilia wakati alipotembelea mabanda ya maonesho ya Biashara mbali mbali mara baada kufungua Tamasha la tatu la Biashara Zanzibar katika viwanja vya Maisara Wilaya ya Mjini Unguja ikiwa ni shamra shamra za miaka 53 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, tarehe 10 Januari, 2017. Kushoto ni Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko Mhe. Amina Salum Ali

Maonesho ya biashara ni utaratibu maalum uliobuniwa na wafanyabiashara miaka mingi iliyopita kwa lengo la kutangaza bidhaa mpya zinazokusudiwa kuuzwa au ambazo ziko tayari kuuzwa kwa watumiaji mbali mbali.

Historia inatufundisha kuwa, maonesho ya kwanza rasmi ya biashara yalifunguliwa nchini Marekani mnamo mwishoni mwa miaka ya 50 karne iliyopita. Maonesho hayo ambayo yameendelea kufanyika katika nchi nyengine nyingi duniani, katika miaka ya karibuni yamekuwa yakitumika siyo tu kuonesha bidhaa mpya zinazozalishwa viwandani, lakini kuuza bidhaa ambazo ziko tayari kwa matumizi.

Kama zilivyo nchi nyengine duniani, wafanyabiashara wa Zanzibar, Tanzania Bara na eneo zima la Afrika ya Mashariki na Kati wamehamisika sana miaka ya karibuni kushiriki katika matamasha ya biashara ili kuuza na kuonesha bidhaa zao.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko imeandaa tamasha la tatu la Biashara mwaka huu kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Maendeleo makubwa ya Sayansi na Teknolojia dunia yanalazimisha mfumo wa matamasha hayo kubadilika kuendana na wakati. Hivyo pamoja na mtindo uliozoeleka wa kuandaa matamasha hayo, ni vyema eneo la Afrika Mashariki na Kati likabuni mbinu mpya za matamasha hayo ya biashara ambazo zitaongeza ufanisi katika kufikia malengo ya matamasha ya biashara.

Akizungumza kwenye tamasha hilo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alisema kufanyika kwa aina hiyo ya matamasha kutaweza kuleta tija na manufaa iwapo yataendeshwa kwa kufuata taratibu na miongozo ya kibiashara na kwamba jambo la msingi ni kuzingatia kuwa na mbinu za kisasa za kutangaza biashara zinazozalishwa hapa nchini.

Katika kufikia azma hiyo wananchi kwa upande wao nao wanao wajibu wa kujenga utamaduni wa kuthamini bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wa ndani ili kuweza kuwapa nguvu katika shughuli zao za uzalishaji.

Imekuwa bahati mbaya sana kwamba wafanyabiashara wengi wanajiingiza kwenye biashara za kununua na kuuza badala ya kuwa

wajasiriamali wanaozalisha bidhaa. Lakini bahati mbaya zaidi nikuona kwamba hata wafanyabiashara wanaofanya bishara za kuuza na kununua wanakuwa wanakosa uaminifu katika biashara hizo wanazozifanya.

Mara kadhaa imeshashuhudiwa baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu wakighushi biashara zao kwa kuweka alama za tarehe bandia na kuuza bidhaa ambazo zimeshapitwa na wakati.

Tunapongeza kauli ya Rais wa Zanzibar aliyoitoa kwenye tamasha hilo kwamba Serkali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejiandaa kuweka mtandao maalum utakaoweza kuwatambua, kuwanasa na kuwafichua wafanyabiashara wanaojaribu kukiuka utaratibu wa kuingiza nchini bidhaa zilizomalizika muda wa matumizi ambayo ni hatari kwa matumizi na maisha ya watumiaji.

Ni dhahiri mipango hiyo ya serikali imekuja baada ya kuongezeka kwa vitendo vya baadhi wa wafanyabiashara kuwa na tabia ya kughushi nembo kwa baadi ya biashara zao zinazoonyesha kuendelea kwa matumizi ya bidhaa hizo kwa kuondosha ile tarehe ya zamani yenye kuonesha kumalizika kwa muda na kuweka tarehe mpya wanazozitaka wao wenyewe huku wakijua kwamba muda wa matumizi ya bidhaa hizo ama unakaribia kumalizika au umeshamalizika kabisa.

Kutokana na serikali ya kuzigundua hadaa hizo zinazofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu hasa bidhaa za vyakula na bidhaa nyengine za matumizi ya binadamu, serikali imewaonya wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa nchini kuacha kutumia mwanya wa kuwepo kwa soko huria kwa kuingiza bidhaa zilizomaliza muda wake.

Vitendo vya aina hiyo vinavyofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu havistahiki kufumbiwa macho na ni lazima hatua kali zichukuliwe dhidi ya wafanyabiashara wote watakaojaribu kukiuka taratibu na maadili ya uendeshaji wa biashara likiwemo tatizo la ukwepaji wa kodi ambalo nalo limekuwa likifanywa na baadhi ya wafanyabiashara wenye tamaa binafsi.

Lakini suala muhimu katika matamasha ya hapa nchini ni kwa wajasiriamali kujitokeza kwa wingi kutangaza bidhaa wanazozizalisha wenyewe badala ya kutegemea bidhaa kutoka nchi za nje ikumbukwe usemi maarufu wa Kiswahili usemao thamini kilichochako mpaka usahau cha mwenzako.

Akizungumza kwenye tamasha hilo, Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Balozi Amina Salum Ali alisema mtazamo wa serikali uliokuwepo hivi sasa ni kutilia mkazo uimarishaji wa viwanda ili viweze kusaidia katika mpango wa mkakati na kuondosha umasikini Zanzibar.

Wakizungumza katika tamasha hilo wafanyabiashara mbali mbali wameelezea kufanyika kwa tamasha hilo kumekuwa kukisaidia kutangaza bidhaa mbali mbali kwa wananchi wanaotembelea katika maonesho hayo.

Tamasha la tatu la biashara limewashirikisha wadau zaidi ya 150 kutoka Zanzibar, Tanzania Bara na Kenya ambapo wafanyabiashara wa aina mbali mbali walipata fursa ya kuonesha bidhaa zao za aina zikiwemo za utoaji huduma za asili.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kutoka kwa Mhandisi Hamis Lusanda (kulia) kutoka Vigor Tp Company Ltd wakati alipotembelea mabanda ya maonesho ya Biashara mara baada ya kufungua Tamasha la tatu la Biashara Zanzibar katika viwanja vya Maisara Wilaya ya Mjini Unguja ikiwa ni shamra shamra za miaka 53 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, tarehe 10 Januari, 2017

# Matukio mbali mbali katika Picha



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na Mwenyekiti wa Kampuni ya Azam Group Bw.Said Salim Bakhresa wakikata utepe kuashiria Uzinduzi wa Mradi wa kiwanda cha uzalishaji wa Maziwa (Azam Dairy Products Ltd.) huko Fumba wilaya ya Magharibi "A" Unguja, tarehe 05 Januari 2017



Rais wa Zanzibar na Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akikata Utepe kuashiria uzinduzi wa Soko la Matunda na Ofisi ya Baraza la Mji la Wete katika shamra shamra za Maadhimisho ya sherehe za miaka 53 ya Mapinduzi Zanzibar, tarehe 28 Januari, 2017. Kulia ni Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na Mwakilishi wa Benki ya Dunia Bibi Elizabeth Ann Talbert wakifungua pazia kuashiria Uwekaji wa jiwe la Msingi jengo jipya la Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Zanzibar huko Mazizini Mkoa wa Mjini Magharibi, tarehe 05 Januari 2017



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akikata utepe kuashiria Uzinduzi wa Vifaa vipya vya kufanyia kazi katika Bandari ya Malindi Mjini Unguja ikiwemo Makontena ya mizigo mizito, uzinduzi huo umefanyika tarehe 04 Januari, 2017

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiangali studio ya Kituo cha Habari ndani ya Skuli ya Sekondari Kwarara mara baada ya kuifungua rasmi, tarehe 11 Januari, 2017





Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akikata utepe ikiwa ni ishara ya ufunguzi wa Skuli ya Sekondari ya Kwarara na Kituo cha Habari, skuli hiyo imejengwa kwa ufadhili wa Serikali ya Korea na imefunguliwa tarehe 11 Januari, 2017. Kulia ni Wafadhili wa Skuli hiyo na Koshoto ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Riziki Pembe Juma na Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Dk. Abdulhamid Yahya Mzee

# Serikali ya Zanzibar haitabinafsisha zao la karafuu




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akinyanyua Nembo ya KARAFUU kama ishara ya Uzinduzi wa Awamu ya kwanza ya Branding ya Karafuu ya Zanzibar,uliofanyika Saateni Mjini Unguja, ikiwa ni shamra shamra za maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, tarehe 06 Januari, 2017

Suala la Serikali kuendelea kuhodhi biashara ya karafuu au kulibinafsisha ili liendeshwe kama ilivyo biashara ya mwani na biashara nyengine za mazao ni suala lililojadiliwa sana miongoni mwa wakulima, viongozi wa vyama, serikali na wananchi kwa jumla na hasa baada ya zao hilo kuonekana kupoteza umaarufu wake wa asili katika soko la ndani na nje ya nchi.

Wazo la kubinafsisha zao hilo ambalo kwa mujibu wa historia ndilo utambulisho wa Zanzibar, lilianzia kwa wafanyabiashara ambao walishaanza kufaidika na biashara ya karafuu waliokuwa wakiifanya kwa njia isiyokuwa rasmi, likaenda kwa taasisi zisizokuwa za serikali NGO zinazojumuisha wakulima wa karafuu ili kujaribu kutumia njia shirikishi za ushawishi, likaingia ndani ya vyama vya siasa ambako lilitumika kama sehemu ya kampeni za kisiasa na hatimaye kufika Serikalini ambako ndiko linakomilikiwa na ambako ndiko kulikofanywa maamuzi.

Licha ya wadau wote walioshiriki hatua za awali kwenye mjadala huo kutaka kubinafsishwa kwa zao hilo, msimamo wa mwisho wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein uliendelea kuwa imara kwa kusisitiza kwamba kamwe zao hilo halitabinafsishwa na kwamba litaendelea kumilikiwa na Serikali kwa manufaa ya taifa na wakulima wa karafuu pamoja na wananchi wote wa Zanzibar.

Msimamo wa Serikali katika suala hilo umezingatia ukweli kwamba karafuu ni zao la kihistoria la taifa na ndio utambulisho wa uchumi wa Zanzibar kwa miaka kadhaa. Aidha, licha ya zao hilo hivi sasa kupata ushindani mkubwa katika soko la dunia kutokana na kuzalishwa na baadhi ya nchi zenye visiwa vilivyopo katika bahari ya Hindi, bado karafuu zinazozalishwa Zanzibar zimekuwa na daraja la juu kutokana na ubora wake na ladha yake ya kipekee, jambo ambalo nchi nyengine zinazozalisha zao hilo kama vile nchi za Mauritius, Shelisheli, Madagascar pamoja na nchi za Malasia, Philippines na Indonesia hazijafikia ubora wa karafuu za Zanzibar.

Kufuatia uamuzi huo, Serikali ya awamu ya saba chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein imelazimika kuchukua hatua mbali mbali za kuliimarisha zao hilo ikiwa ni pamoja na kulifanyia marekebisho makubwa Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) ili liweze kujiendesha kibiashara, pamoja na kuifanyia utambulisho maalum karafuu ya Zanzibar, hatua ambayo itaondosha uwezekano wa watu wengine kuighushi na kuharibu umaarufu wake.

Wakulima wa karafuu wameendelea kulipwa TZS 14,000 kwa kilo moja, ikiwa ni sawa na asilimia 80 ya bei ya soko ya kuuzia nje. Katika mwaka 2015/16, ZSTC ilinunua tani 5,764.8 za karafuu, kwa TZS bilioni 80.9 Katika mwaka 2015/16, ZSTC iliuza nje ya nchi, jumla ya tani 5667 za karafuu, zenye thamani ya USD milioni 45.63, sawa na TZS bilioni 98.2. Kadhalika, Shirika limeuza nje ya nchi mafuta ya viungo yenye thamani ya TZS milioni 872.37 katika mwaka 2016.

Kadhalika katika kipindi hicho Serikali imeendelea na utaratibu wake wa kuwapa wakulima wa karafuu miche ya mikarafuu bure, kwa lengo la kuliendeleza zao hilo. Jumla ya miche 450,540 ya mikarafuu ilitolewa Unguja na Pemba. Vile vile, maandalizi ya Mkakati wa Tasnia Malibunifu (Branding), kwa karafuu za Zanzibar na viungo vyengine yalikamilishwa na majaribio yake yamezinduliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein tarehe 6 Januari, 2017.

Akizungumza katika uzinduzi wa awali wa `Brading` ya karafuu na viungo vyengine huko Saateni katika shamra shamra za kutimia miaka 53 ya Mapinduzi ya Zanzibar Dk. Shein alisema Zanzibar itaendelea kulitambua zao la karafuu kuwa zao kuu la taifa na ndio maana juhudi zinachukuliwa katika kuliimarisha zao hilo ikiwemo hatua ya kulitafutia utambulisho maalum kwa lengo la kuijengea hadhi karafuu hiyo katika soko la kimataifa ambako Zanzibar imekuwa ikikabiliana na ushindani baina yake na nchi nyingine zinazozalisha karafuu.

Pamoja na juhudi hizo zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kulijengea thamani hilo kitaifa na kimataifa bado kumekuwa na watu wanaojaribu kufanya magendo ya karafuu kwa kutumia hadaa mbali mbali kutaka kuzivunjia hadhi na ubora wake kutokana na tamaa zao binafsi.

"Hatutakuwa tayari kuwaachia watu wachache wa aina hiyo wenye lengo la kutuharibia karafuu zetu ambazo ndio tegemeo kubwa la uchumi wa taifa letu" alisisitiza Dk. Shein

# Mkanyageni yapata Skuli ya Sekondari ya kisasa

- Yapewa jina la mmoja wa waasisi wa Mapinduzi - Mohamed Juma Pindua

Jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuimarisha sekta ya Elimu zinazidi kuonekana katika kila eneo Unguja na Pemba kufuatia kuweko na matukio tofauti ya uzinduzi wa miradi mipya mikubwa ya elimu na mingine kuwekwa mawe ya msingi katika maadhimisho ya sherehe za miaka 53 ya Mapinduzi Zanzibar na hata kabla ya hapo.

Matukio ya hivi karibuni kabisa ya miradi ya elimu yaliyomhusisha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kuadhimisha miaka 53 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ni pamoja uzinduzi wa Skuli mpya ya kisasa katika kijiji cha Mkanyageni ilyopewa jina la mmoja wa waasisi wa Mapinduzi - Mohamed Juma Pindua na Skuli ya Sekondari ya Kwarara ambazo zote zimejengwa kwa kiwango kinachokubalika na zinaonekana kuwa za kisasa kwa majengo na vifaa vilivyomo. Matukio hayo mawili yanazidi kuwathibitishia wananchi dhamira ya kweli ya serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo yao.

Kukamilika kwa ujenzi wa skuli ya Sekondari ya Mohamed Juma Pindua siyo tu itasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi kwenye skuli za Sekondari zilizo karibu na eneo hilo, lakini pia kunatoa fursa kwa wananchi wa kijiji cha Mkanyageni na maeneo mengine ya Pemba kuondokana na usumbufu waliokuwa wakiupata kabla ya kuwepo kwa skuli hiyo



Jengo jipya la Skuli ya Sekondari ya Mkanyageni iliyopewa jina la Mohamed Juma Pindua katika Kijiji cha Mkanyageni Mkoa wa Kusini Pemba, lililozinduliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika shamra shamra za maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, tarehe 07Januari 2017

na hivyo kuongeza ufanisi wa wanafunzi katika masomo yao.

Kuenea kwa huduma za elimu katika ngazi zote kunahesabika kuwa ni kufaulu kwa malengo ya Mapinduzi ambayo miongoni mwa malengo yake makuu yalikuwa ni kuwapatia wananchi huduma ya elimu bure na bila ya aina yoyote ya ubaguzi.

Ujenzi wa Skuli hiyo ni miongoni mwa ahadi alizozitoa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein tokea awamu ya kwanza ya uongozi wake. Ujenzi wa Skuli hiyo ulianza ndani ya kipindi chake cha kwanza cha uongozi na imejengwa na kampuni inayomilikiwa na wazalendo.

Akizungumza na wananchi na viongozi mbali mbali waliohudhuria hafla ya ufunguzi wa hospitali hiyo, Dk. Shein aliwataka wananchi wa Mkanyageni na maeneo jirani ya Pemba kuitumia vyema skuli hiyo kuwasomesha watoto wao masomo ya aina mbali mbali kwani alisema fursa ya elimu ilikuwa haipatikani kwa wanyonge wakati wa ukoloni na ndio miongoni mwa sababu za kufanywa Mapinduzi.

Alisema wananchi wote wanayo kila sababu ya kujivunia mafanikio yaliyopatikana baada ya Mapinduzi kwani yamewaondolea maisha ya matabaka na kuwawezesha watoto wa wanyonge kuweza kupata elimu bure ambayo ndiyo yaliyokuwa miongoni mwa malengo makuu ya Mapinduzi.

Alisema kutokana na mafanikio hayo ipo haja ya kuyatunza na kuyaenzi Mapinduzi Matukufu ya Januari tarehe 12,1964 ambayo yameondosha madhila mbali mbali ikiwemo ya ukoloni pamoja na utumwa na kuwafanya wananchi wa Zanzibar kuwa huru kwenye ardhi yao.

Dk. Shein alisisitiza kwamba ili dhana hiyo iweze kuendelea na kurithiwa na vizazi vijavyo, wazee wazalendo hawanabudi kuwafundisha historia vijana wao ili waweze kuijua nchi yao inakotoka, ilipo na iendako.

Vile vile katika hotuba yake kwa maelfu ya wananchi waliohudhuria kilele cha maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alibainisha mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta ya elimu nchini akitoa takwimu za mwaka mmoja uliopita.

"Leo hii Mkanyageni imebadilika na kila mmoja wetu anaona mafanikio hayo. Zote hizo ni juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa C.C.M na kuwabeza wale wanaoponda mafanikio hayo" alisema Dk. Shein.

Katika mwaka 2016, idadi ya skuli imeongezeka kutoka 792 mwaka 2015 hadi 843, sawa na ongezeko la asilimia 7. Idadi ya wanafunzi walioandikishwa, nayo imeongezeka kutoka wanafunzi 388,616 mwaka 2015 hadi kufikia 424,074 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 8.36. Kiasi hicho ni kikubwa sana ikilinganishwa na hali halisi ya sekta ya elimu kabla ya Mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964.

Kwa lengo la kuondoa msongamano wa wanafunzi katika skuli za sekondari, ukiachilia miradi ya Skuli za Sekondari zilizokwisha kufunguliwa, Serikali imeshakamilisha michoro ya ujenzi wa skuli 9 za ghorofa zitakazojengwa katika Wilaya ya Mjini, Magharibi A na B kwa Unguja na Wilaya zote nne za Pemba. Fedha za ujenzi huo tayari zimepatikana kutoka Benki ya Dunia.

Aidha, vituo viwili vipya vya mafunzo ya amali vimeanza kujengwa huko Makunduchi, Unguja na Daya Mtambwe, Pemba kwa mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Vile vile, jengo jipya la Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia litakalokuwa na madarasa, maabara na karakana limeanza kujengwa na jiwe la msingi liliwekwa rasmi tarehe 8 Januari, 2017 na linatarajiwa kukamilika, mwezi wa Mei, 2017.

Vile vile mafanikio makubwa yamepatikana katika kuimarisha elimu ya juu. Idadi ya wanafunzi wanaosoma elimu ya juu katika vyuo vikuu vya Zanzibar imeongezeka, kutoka wanafunzi 6,370 mwaka 2015 hadi kufikia 7,383 mwaka 2016, ongezeko hili ni sawa na asilimia 5.9.

Katika kupanua fursa za elimu ya juu, Serikali imekiunganisha Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na Chuo cha Utalii Maruhubi, Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka pamoja na Chuo cha Sayansi za Afya Mbweni, ili vyuo hivyo vilivyoounganishwa viweze kuwa na fursa ya kutoa elimu ya juu na kuongeza idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Kuhusu mikopo ya elimu ya juu, Serikali imetoa mikopo kwa wanafunzi 2,655 na jumla ya TZS bilioni 3.7 zimetolewa kwa ajili ya wanafunzi hao. Kadhalika, Serikali imekusanya jumla ya TZS milioni 480 kutoka kwa wahitimu waliorudisha mikopo, kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Kwa ujumla hali ya elimu Zanzibar ndani ya miaka 53 baada ya Mapinduzi imeimarika zaidi ikilinganishwa na zaidi ya miaka 250 walioishi wananchi wa Zanzibar chini ya utawala wa kikoloni, ambao kwa mujibu wa historia waliacha skuli mbili tu za maandalizi na 62 tu za msingi, kulikuwa na skuli nne tu za sekondari na hakukuwa na hata chuo kikuu kimoja.

Hali hiyo ni tofauti na sasa ambapo idadi ya skuli katika ngazi ya elimu ya lazima zimefikia zaidi ya 800 mpaka kufikia mwaka 2016. Kwa upande wa Pemba hadi mwaka 1963 kulikuwa na skuli 21 ikiwa ni pamoja na skuli moja ya sekondari ya Fidel Castro. Hadi kufikia mwaka jana skuli za serikali kisiwani Pemba zimefikia 184 na sekondari zilikuwa 61 baada ya kufunguliwa skuli mpya ya Sekondari ya Abdalla Pindua sasa zitakuwa 62.

Ni ukweli uliowazi kwamba iwapo vijana wataweza kuijuwa vyema historia ya nchi yao pamoja na kutambua kilichosababisha kufanyika Mapinduzi, wataweza kuwapuuza baadhi ya watu wachache ambao wamekuwa wakiyabeza Mapinduzi hayo hali ya kwamba ndiyo yaliyowalea na kuwafikisha hapo walipo.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiangalia vitabu wakati alipotembelea madarasa na maabara mara baada ya kuizindua Skuli Mpya ya Sekondari ya Mohamed Juma Pindua katika Kijiji cha Mkanyageni ikiwa ni shamra shamra za maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, tarehe 07Januari 2017. Kushoto ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Riziki Pembe Juma

# Wananchi wafurahia mradi wa skuli, kituo cha habari - Kwarara

Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki ni msemo maarufu wa Kiswahili ambao umekuwa ukitumika katika matukio tofauti kwa watu kufarijiana hasa baada ya mmoja kati ya wahusika kutoka kwenye majonzi makubwa yaliyomsibu kwa muda maalum.

Hii ndiyo hadithi ya Serikali ya Zanzibar pamoja na wananchi wa Kwarara, wanavyowazungumzia ndugu zao wa Korea ambao wamesaidia ujenzi wa skuli ya kisasa ya Sekondari ya Kwarara na kituo cha habari kilichozinduliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika shamra shamra za maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mradi wa ujenzi wa Skuli hiyo umekuja wakati ambapo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imo katika jitihada za kupanua wigo wa nafasi za masomo kwa wanafunzi wa Mkoa wa Mjini Magharibi, kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi ndani ya Mkoa huo na hivyo kusababisha mrundikano mkubwa wa wanafunzi kwenye skuli za Sekondari ndani ya Mkoa huo.

Kwa mujibu wa hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa kwenye kilele cha maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika mwaka 2016, idadi ya




Jengo la Skuli mpya ya Sekondari ya Kwarara na Kituo cha Habari, iliyofunguliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein iliyojengwa kwa ufadhili wa Serikali ya Korea. Ufunguzi huo umefanyika tarehe 11 Januari, 2017

skuli imeongezeka kutoka 792 mwaka 2015 hadi 843, sawa na ongezeko la asilimia 7. Idadi ya wanafunzi walioandikishwa, nayo imeongezeka kutoka wanafunzi 388,616 mwaka 2015 hadi kufikia 424,074 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 8.36.

Kwa lengo la kuondoa msongamano wa wanafunzi katika skuli za sekondari, Serikali imeshakamilisha michoro ya ujenzi wa skuli 9 za ghorofa zitakazojengwa katika Wilaya ya Mjini, Magharibi A na B kwa Unguja na Wilaya zote nne za Pemba. Fedha za ujenzi huo tayari zimepatikana kutoka Benki ya Dunia.

Wataalamu wa masuala ya maendeleo wamethibitisha kuwa msaada pekee wenye manufaa makubwa kwa binadamu ni msaada wa elimu ikiwa ya dunia au ile ya akhera. Elimu siyo tu inamuwezesha mtu kutoka kwenye ujinga, lakini inampa uwezo binadamu yeyote kuwa na mipango ya uhakika na kuweza kufikiria sababu ya kila tukio linalojiri katika mwenendo wa maisha yake.

Wazee wenye elimu na busara wanaamini kwamba urithi mkubwa wa kuwaachia watoto wao ni elimu ambayo kamwe hakutakuwa na mtu ambaye atathubutu kuipora hata baada ya wazazi kuondoka duniani. Lakini waswahili wamesema pia ukitaka kumsaidia mtu mwenye hamu ya kula samaki, ni vyema ukamfundisha namna ya kuvua samaki na kumpa nyenzo za kuvulia badala ya kumpa



Jengo la Skuli mpya ya Sekondari ya Kwarara na Kituo cha Habari, iliyofunguliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein iliyojengwa kwa ufadhili wa Serikali ya Korea. Ufunguzi huo umefanyika tarehe 11 Januari, 2017

samaki mwenyewe ambaye atamtumia mara moja.

Kutokana na ukweli huo ndio maana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akaipongeza Serikali ya Jamhuri ya Korea kupitia Mashirika yake kwa kuendelea kuiunga mkono Zanzibar katika sekta za maendeleo ikiwemo sekta ya elimu kutokana na ukweli kwamba elimu ndio ufunguo wa maisha.

Jamhuri ya Korea kupitia Mashirika yake imeendelea kuiunga mkono Zanzibar katika harakati za kuleta maendeleo hapa Zanzibar na kwamba mradi wa skuli ya Kwarara na Kituo cha habari chini ya ufadhili wa Shirika la Habari la mjini Seoul Seoul – "Broadcasting System (SBS TV)" ni mradi wa mwanzo wa aina yake katika miradi ya elimu.

Aidha, Serikali ya Korea kupitia Shirika lake la Good Neighbors Tanzania imekubali kujenga skuli ya msingi huko Kwarara itakayokuwa na madarasa 24 ambapo tayari eneo la skuli hiyo limeshapatikana.

Sambamba na hayo, Shirika la KOICA linatarajia kutoa msaada wa dola za Kimarekani milioni 10 ambazo zitapitia Shirika lisilo la Kiserikali la Korea kwa ajili ya kuimarisha elimu ya Sekondari kwa wanafunzi wa kike.

KOICA imeahidi kuunga mkono miradi mengine mipya itakayoianzisha hapa Zanzibar ikielezea kuridhishwa kwake na mashirikiano mazuri wanayoyapata kutoka kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mafanikio ya ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Kwarara umefanikiwa kutokana na wananchi wa eneo hilo kuunga mkono kwa dhati jitihada za serikali za kuleta maendeleo. Wazee wawili wa familia moja Bwana Mohamed Salum na Bwana Ali Salum wanaomiliki shamba ndani ya eneo lililojengwa skuli hiyo ambao wamekubali kwa hiari yao kutoa sehemu ya ardhi ndani ya shamba lao ili kutoa fursa ya kutekelezwa mradi huo.

Moyo huo wa kijasiri uliooneshwa na wazee hao wawili ni tofauti na baadhi ya wananchi kwenye maeneo mengine, ambako imeshindikana kupelekwa miradi mikubwa ya maendeleo waliyoiomba wenyewe serikalini kwa maslahi yao baada ya kutakiwa kusamehe fidia kwa maeneo ambayo huenda yakaathirika kutokana na mradi husika.

Uongozi wa KOICA umetoa pongezi maalum kwa Dk. Shein kwa mafanikio makubwa yaliofikiwa Zanzibar katika kipindi kifupi na kuahidi kuendelea kuiunga mkono Zanzibar katika kuimarisha sekta za maendeleo ikiwemo sekta ya elimu.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiangali studio ya Kituo cha Habari ndani ya Skuli ya Sekondari Kwarara mara baada ya kuifungua rasmi, tarehe 11 Januari, 2017




Jengo jipya la Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Zanzibar, lililowekewa Jiwe la Msingi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein linaloendelea kujengwa Mazizini Mkoa wa Mjini Magharibi, Jiwe hilo limewekwa tarehe 06 Januari, 2017

# SMZ Yahimiza Matumizi ya Takwimu Sahihi kwa Maendeleo Endelevu

Matumizi ya takwimu sahihi katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo ni jambo la lazima katika nchi au taasisi yoyote inayokusudia kuwa na maendeleo endelevu.

Zanzibar ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama zilivyo nchi nyengine duniani, imekuwa ikichukua juhudi mbali mbali za kuimarisha mfumo wake wa takwimu, ili kuhakikisha kuwa mipango yake inakuwa sahihi siyo tu katika kupanga, lakini pia katika kuifanyia tathmini kwani takwimu hizo ndizo zitakazoweza kutoa hali halisi kabla ya utekelezaji wa miradi husika, wakati wa utekelezaji na pia baada ya utekelezaji.

Uamuzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya saba wa kutumia



takwimu kama taarifa muhimu katika mipango ya maendeleo, unaenda sambamba na uamuzi wa kuanzisha Idara za Mipango sera na Utafiti katika kila Wizara ya Serikali.

Hivyo uamuzi huo ulionekana kuwa ni hatua ya lazima kwani takwimu sahihi zinapatikana katika taarifa zilizofanyiwa utafiti wa kina na zinakuwa ndio msingi au chanzo cha tafiti nyengine zitakazofanyika siku zijazo.

Katika kulitilia mkazo suala hili Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein wakati wa kikao cha kutathmini utekelezaji wa mpango kazi, aliiagiza Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kukaa pamoja na Tume ya Mipango pamoja na ofisi ya Mtakwimu mkuu wa Serikali kuangalia utaratibu bora zaidi wa kuratibu shughuli za utafiti hasa baada ya Zanzibar kuwa na mpango wake wa utafiti ambao umeainisha maeneo yake ya utafiti na vipaumbele vyake.

Katika kufanikisha mpango huo amesema kuwa kuna haja ya kuwekwa mfumo mathubuti katika kuondoa hitilafu kutokana na kuwepo kwa tatizo la ukusanyaji, utumiaji na uhifadhi wa takwimu hapa nchini

Wito huo wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi umekuja kutokana na changamoto zilizopo katika kutafuta, kupata na hatimaye kutumia takwimu. Imeshawahi kutikezea mara kadhaa taasisi moja kutoa takwimu tofauti. Hali kama hiyo inapotokea kwenye taasisi, basi taarifa zote za taasisi hiyo zinakuwa haziaminiki hasa zinapokwenda kwa watu wenye kuzifanyia kazi takwimu na kufahamu umuhimu wake.

Akizungumza mara baada ya kuweka jiwe la msingi la Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa serikali iliyoko Mazizini Mjini Unguja katika shamrashamra za miaka 53 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alisema bila ya kuwepo mfumo mzuri wa kitaalamu wa ukusanyaji wa takwimu, Serikali haitoweza kuwa na taarifa sahihi na hivyo kusababisha wananchi kukosa taarifa sahihi za serikali ambazo ni haki yao ya kikatiba.

"Mimi mwenyewe ni mtumiaji mkubwa wa takwimu, lakini unapohitaji takwimu kutoka Wizarani basi kwa wakati mmoja tarajia kupata takwimu tofauti" alisema Dk. Shein.

Katika maelezo yake, Dk. Shein alisema kuwa udhaifu katika utoaji wa takwimu na taarifa, ni ukiukaji wa maadili ya uongozi na utumishi wa umma. Hivyo alitoa wito kwa kila Wizara kuhakikisha kuwa inakuwa na mtaalamu wake wa takwimu katika Idara ya Mipango na Sera ambaye pia atakuwa ndiye kiungo baina ya Wizara na Ofisi ya Mtakwimu mkuu wa Serikali.

Alisisitiza haja ya kubadilika kwa kuondokana na utaratibu uliopo hivi sasa wa kila mmoja kuwa na mamlaka ya kutoa takwimu za Serikali na badala yake kufuata taratibu za Serikali katika utoaji wa takwimu. Sambamba na hatua hiyo ameitaka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuandaa utaratibu mzuri wa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu takwimu pamoja na umuhimu wa takwimu.

Aidha, ameitaka Wizara ya Fedha na Mipango kuongeza kasi ya kuwasomesha wafanyakazi wanaohusika na takwimu, ili kupatikane wataalamu wa kutosha, watakaoweza kukusanya na kutoa tafsiri za takwimu na uhusiano wake na maendeleo.

Kutokana na umuhimu wa takwimu Dk. Shein alieleza azma ya Serikali kutoa semina maalum kwa viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa lengo la kuelewa suala zima la takwimu na hatimae kusaidia kufanya kazi kwa haraka na kwa ufanisi zaidi.

# Pemba washerehekea Mapinduzi kwa vifijo na nderemo



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Nd. Radhiya Rashid kuhusu Soko la Matunda na Ofisi ya Baraza la Mji Wete Mkoa wa Kaskazini katika Shamra shamra za Maadhimisho ya miaka 53 ya Mapinduzi Zanzibar, tarehe 08 Januari, 2017

Wananchi kisiwani Pemba wamesherehekea sherehe za maadhimisho ya kutimiza miaka 53 ya Mapinduzi ya Januari 1964 kwa furaha kubwa na nderemo wakichanganya maadhimisho hayo na kukamilika kwa miradi ya kuimarisha huduma za jamii mijini, ambayo moja kwa moja inatoa faida nyingi kwa wananchi.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein imeendelea vyema na utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020 kwa kutekeleza miradi mikubwa ya kiuchumi na kijamii na kuiwezesha Zanzibar kuendelea kupiga hatua zaidi za kimaendeleo.

Miongoni mwa miradi mingi iliyoweza kufanikiwa chini ya uongozi wa Dk. Shein na kuweza kuleta faraja na matumaini makubwa kwa wananchi wa Unguja na Pemba, ni mafanikio ya mradi wa Huduma za jamii mijini ZUSP.

Mradi huo wa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ulioanzishwa mwaka 2015, unatokana na mkopo wa Benki ya Dunia wa Dola milioni 38 za Marekani ambazo kwa wakati huo zilikuwa karibu shilingi bilioni 56 za Tanzania na zilitengwa kwa ajili ya mradi wa kuimarisha huduma za jamii mijini yaani - Zanzibar Urbarn Service Project uliosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango na kuendeshwa na



Soko la Matunda la Mji wa Wete, Pemba

Baraza la Manispaa Zanzibar na Halmashauri za Wilaya ya Wete, Mkoani na Chake chake.

Mtazamo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa kuanzisha miradi hiyo ni kuimarisha huduma zilizokuwa bora zaidi kwa lengo la kuiweka miji hiyo kuwa ya kisasa zaidi kwa kuimarisha mipango miji na usafi wa mazingira katika maeneo hayo.

Kutokana na umuhimu wa mradi huo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa kipindi chote cha utekelezaji wake alikuwa karibu kufuatilia utekelezaji wa mradi huo ili kufahamu na kuona jinsi kazi za mradi huo zinavyoendelea akifahamu umuhimu wake kwa wananchi kiuchumi na kimazingira.

Miradi hiyo ya Huduma za jamii Mjini iliyopata fursa ya kuitembelewa na Dk. Shein wakati imo katika utekelezaji wake, ni ujenzi wa ukuta wa Forodhani, Matengenezo ya Ofisi kuu ya Manispaa iliyopo Malindi na ujenzi wa mtaro wa maji ya mvua uliopo Mnazi mmoja na mradi utakaowekwa taa za njiani kwa kutumia umeme wa sola huko Saateni.

Katika mazungumzo yake kwenye sherehe za uzinduzi wa soko la Wete katika shamrashamra za kuadhimisha miaka 53 ya Mapinduzi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliwataka wananchi wa Wete kulitumia soko hilo vizuri na kufanya kazi kwa bidii ili kukabiliana na changamoto za maisha ikiwamo umasikini.

Amesema Serikali itaendelea kutekeleza wajibu wake wa kuwatumikia wananchi wote bila ya ubaguzi kwani malengo ya Mapinduzi yalikuwa ni kuwakomboa wananchi wote wa Zanzibar bila ya ubaguzi kutoka katika utawala wa kidhalimu ambao kamwe hautorudi tena.

Katika mahojiano maalum na wananchi mbali mbali wa miji ya Mkoani, Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba wameipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuweza kufanikisha miradi ya uimarishaji wa miji kupitia Mradi wa Huduma za jamii mjini ZUSP na hivyo kuuwezesha mji huo kuwa na mabadiliko makubwa.

Walisema kumalizika kwa miradi hiyo na kuweza kufunguliwa kwenye shamra shamra za kutimia miaka 53 ya Mapinduzi na Waziri wa Fedha Khalid Salum kunastahili kupongezwa kwani miradi hiyo mbali ya kuijengea haiba mji huo lakini kutaweza kuwanufaisha wananchi waliowengi kiuchumi na kimaendeleo.

Walisema miradi hiyo kwa mara nyengine tena imethibitisha dhamira ya kweli ya Serikali katika kuwaletea maendeleo yao na imefuta dhana ya wapinga maendeleo ambao mara zote wamekuwa wakibeza na kukebehi ahadi zote zilizokuwa zikitolewa na serikali kwa wananchi wakinasibisha ahadi hizo na mchezo wa siasa.

"Mimi ni Diwani wa Wadi ya Makoongwe kupitia chama cha Mapinduzi na katika Halmashauri yetu ya Wilaya ya Mkoani wajumbe wengi walikuwa kutoka upande wa upinzani,hivyo tulipokuwa tukiinadi miradi hii tulilazimika kufanya kazi ya ziada kwani wajumbe wezentu walikuwa wakiona kuwa ni propaganda za kisiasa na hakuna chochote kitakachofanyika, sasa nashukuru Mungu ukweli umejidhihirisha kwa kuwa miradi hiyo ipo na inaonekana" alisema Diwani wa Makoongwe.

Naye Bw. Haji Khamis Haji mfanyakazi wa Baraza la Mji Mkoani amesema kumalizika kwa miradi mitatu chini ya mradi wa ZUSP ukiwemo ukarabati wa ujenzi wa ofisi ya Baraza la Mji Mkoani kumeweza kuongeza wingi wa nafasi kwa wafanyakazi wake ambapo hapo awali kulikuwa na uchache wa nafasi na hivyo kusababisha msongomano wa kiutendaji kwa wafanyakazi.

"Nashindwa kuelezea furaha yangu kutokana na kumalizika kwa ukarabati wa jengo letu hili la Baraza la mji Mkoani, mbali ya uzuri wa haiba yake lakini sasa wafanyakazi wanazo nafasi za kutosha ambapo kila kitengo kina ofisi na vifaa vya kufanyia kazi kwa nafasi" alisema Bw. Haji Khamis.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Mhe. Rashid Ali Juma, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein, Waziri Mkuu wa Tanzania Mhe. Kasim Majaliwa Majaliwa, Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi pamoja na wake wa viongozi wakiwa katika Ukumbi wa zamani wa Baraza la Wawakilishi katika Taarab rasmi ya kusherehekea Miaka 53 ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyofanyika tarehe 12 Januari, 2017

# Kikundi cha Taifa cha Taarab kilivyokonga nyoyo za wananchi

Taarab rasmi iliyotumbuizwa na Kikundi cha Taifa ilikuwa ni miongoni mwa shamra shamra ya sherehe za Mapinduzi matukufu ya miaka 53 kwa mwaka huu. Onesho la taarab hiyo lilifanyika katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi la zamani liliopo Kikwajuni Mjini Unguja ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alikuwa mgeni rasmi.

Katika taarab hiyo jumla ya nyimbo 14 zenye maudhui mbali mbali yakiwemo yale yenye mnasaba na sherehe hizo yaani kumbukumbu ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, nyimbo za kuhamasisha kuilinda amani ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla wake, nyimbo ya pongezi maalum kwa Dk. Shein kwa jitihada zake za kuiletea maendeleo Zanzibar bila kusahau mashairi mbali mbali ya mafumbo yaliowaacha mashabiki wa mziki huo kila mmoja kutafsiri kwa namna aonavyo yeye mwenyewe.

Vinanda vilivyopangwa na kucharazwa kwa ueledi na ustadi mkubwa pamoja na sauti maridhawa za waimbaji kutoka ndani ya kikundi hicho viliweza kukonga nyoyo za waliohudhiria hafla hiyo na wengine kushindwa kujizuia na kujikuta wakitikisa vichwa au kunyanyuka kwenda kutunza ikiwa ni ishara ya kuonesha kuguswa na burdani hiyo.

Kikundi hicho kilianza na wimbo wa Amenipokea ulioghaniwa na mwimbaji Sheria Issa, wimbo uliobeba maudhui ya Miaka 53 ya Mapinduzi uliimbwa na Bibie Hilda Mohd, nae Al - Anisa Sabina Hassan alikuja na kibao chake maridhawa kinachojulikana kwa jina la Nimtakae Hataki.

Mwenyekiti wa Kikundi hicho Ndugu Iddi S. Suwedi nae alipanda na kibao chake kilichobeba ujumbe wa Tuilindeni Amani, wimbo huu ulikuwa ni kati ya nyimbo zilizotegewa sikio na Mgeni rasmi Dk. Ali Mohamed Shein kutokana na mashairi yake yaliyokuwa yakihimiza umuhimu wa watanzania kuilinda amani ya nchi yetu. Miongoni mwa beti zinazopatikana ndani ya wimbo huo ni kama hii ifuatayo.

Tusifanye masihara
Amani kuichezea
Amani si wera wera
Yafaa kuzingatia
Umakini na ubora
Amani kusimamia
Haitakiwi papara
Amani kuivamia.




Mgeni rasmi Dk. Ali Mohamed Shein pamoja na viongozi wengine wa Serikali zote mbili akiwemo Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, walionekana kutulia kwa mda mrefu wakifuatilia kwa umakini mashairi na vinanda vilivyokuwa vikirindima ndani ya ukumbi huo wakati wake wa viongozi Mhe. Mama Mwanamwema Shein pamoja na Mhe. Mama Asha Suleiman Iddi wao walionekana wakisimama mara kwa mara na kwenda kutunza huku wakisindikizwa na kundi la mashabiki walionekana kuinogesha vyema hafla hiyo.

Wimbo wa Kama Yalivyonipata uliimbwa na Bibie Maryam Juma kabla kupanda kwa Mamaa wa Minenguo Saada Nassor kuwasilisha wimbo Wahoi, nyimbo hii ya Wahoi ilitumbuizwa kutokana na Mapendekezo ya Mke wa Rais wa Zanzibar Mhe. Mama Mwanamwema Shein na ni miongoni mwa nyimbo zilizovuma miaka ya nyuma ikiimbwa na Malkia wa Mipasho Bibie Khadija Omar Kopa, suala lililokuwa likiulizwa ndani ya nyoyo za mashabiki ni kiasi gani Bibi Saada Nassor ataweza kuumudu wimbo huo lakini suala hilo lilipata jibu mara tu iliposikika sauti yake kwani alionesha umahiri na ustadi wa hali ya juu mda wote aliposimama mbele ya jukwaa.

Lulu ni jina la nyimbo iliyopata bahati kusikika katika hafla hiyo ambayo ilighaniwa na Ustadh Khamis Nyange (Profesa Gogo) kutoka Kisiwani Pemba, nayo sauti nyororo na laini ya Bibie Rukia Ramadhan ilivuma ndani ya ukumbi huo na wimbo wake Njoo kwa Mtu Mkweli na kuudhihirishia umma kuwa kweli vya kale ni dhahabu. Kiongozi wa Kikundi hicho Ndugu Mohd Ilyas yeye alipanda kwa awamu mbili tofauti ya kwanza akiimba wimbo unaojulikana kwa jina la Muungwana na wimbo wa pili ambao ulikuwa ni wa mwisho kabisa katika hafla hiyo unajulikana kwa jina la Hofu yako iondoe. Mkongwe huyu wa mziki huu wa taarab hapa nchini alitumia mda wake vyema kwa kughani na kusarifu sauti yake hali iliyosababisha kuwainua mashabiki mara kwa mara juu ya viti vyao.

Tukio lililobeba hisia ndani ya hafla hiyo na wengi likawafurahisha ni pale Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaaliwa alipojisikia kutaka kutunza lakini kutokana na jukwaa kuzongwa na mashabiri mara zote kila nyimbo inapoanza kupigwa aliamua tunza yake ya Dola 200 za Kimarekani kumkabidhi Mshauri wa Rais wa Masuala ya Utamaduni na Utalii ndugu Chimbeni Kheri kuiwasilisha kwa Kikundi cha Taifa.

Dk. Ali Mohamed Shein alionekana tena kutulizana na kusikiliza kwa umakini zaidi wimbo uliotajwa kwa jina la Rais Twakupa Pongezi, wimbo ambao uliyataja wazi wazi baadhi ya mambo yaliyotekelezwa na Dk. Shein na ambayo yaliyowakuna wazanzibari wengi kama vile kuanzisha Pencheni Jamii kwa Wazee, Kuimarisha Sekta ya Utalii, na kubwa zaidi ni suala la Amani na Utulivu wa Zanzibar. Wimbo huu ulighaniwa na waimbaji wanne tofauti ambayo ni Bibie Saada Nassor, Asha, Maryam na Sabina Hassan.

